
# Unachohitaji kujua kuhusu vizuizi kwenye msaada wa afya ya kimataifa wa marekani:

## Sera Ya Kulinda Maisha Katika Msaada Wa Afya Ya Kimataifa

Mwongozo Usio Rasmi



PAI
pai.org

Novemba 2020

### Kuhusu PAI

PAI inafanya utetezi na watungaji wa sera huko Washington D.C na mtandao wa washirika wetu wa kimataifa na wafadhiliwa ili kuendeleza haki za afya ya kijinsia na uzazi kwa kuondoa vizuizi vya sera na ufadhili. PAI, ambayo ilianzishwa mwaka wa 1965, ni kundi binafsi lisilotengeneza faida nalo halikubali fedha za serikali.

### Kanusho

Kwa niaba ya PAI, bodi yake ya wakurugenzi na wafanyakazi: Hakuna taarifa yoyote iliyo katika mwongozo huu inayopaswa kutafsiriwa kama uungaji mkono wa waziwazi au usio wa waziwazi wa sera ya Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa au utekelezaji wake na serikali ya Marekani.

Maudhui ya mwongozo huu yamekusudiwa kuwasilisha taarifa za jumla tu nayo si ushauri wa kisheria. Ushauri wa kisheria bila malipo unapatikana. Tafadhali wasiliana na PAI ili uunganishwe na mawakili walio tayari kuyashauri mashirika kuhusu sera ya Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa.

Ili kupata nakala za hati zilizonukuliwa au kurejelewa katika mwongozo huu, omba msaada wa kuelewa sera za sasa za serikali ya Marekani au shiriki uzoefu wa shirika wa kutekeleza sera ya Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa, tafadhali wasiliana na PAI kwa barua pepe kupitia PLGHA@pai.org au kwa simu +1 (202) 557-3400. Kwa taarifa zaidi, tembelea www.pai.org.



## Yaliyomo


**Utangulizi** 4

**Muhtasari wa *Sera*** 5

**Msamiati wa Kisheria wa *Sera*** 7

- "Ukaguzi wa Miezi Sita" 7
- Vipengele vya Kawaida Vilivyorekebishwa 7

**Wakati wa Kutekelezwa** 8

- Fasiri ya Mei 2019 8

**Wigo wa *Sera*** 9

- Mashirika na Taasisi 10
  - Yanayodhibitiwa na *Sera* 10
  - Yasiyodhibitiwa na *Sera* 10
    - Mashirika 10
    - Wafanyakazi wa Mashirika 10
    - Serikali Ambazo Si za Marekani 10
    - Mashirika Ya Kimataifa 11
- Shughuli 11
  - Uavyaji Mimba 11
  - Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba 11
  - Ushawishi Kuhusu Uavyaji Mimba 11
  - Utunzaji Baada ya Uavyaji Mimba 12
    - Mafunzo na Vifaa 12
    - Ushauri na Huduma za Kuzuia Mimba 12
  - Utafiti Kuhusu Uavyaji Mimba 12
    - Utafiti wa Tiba ya Biolojia 12
    - Utafiti wa Kidemografia na Afya 12
    - Utafiti wa Mipango na Uendeshaji 12
  - Msaada wa Kiufundi 12
- Majukumu ya Utiifu na Ufuatiliaji 13

**Taarifa Zaidi** 14


## Orodha ya Vielelezo


Kielelezo cha 1: Shughuli Zinazohusiana na Uavyaji Mimba Zinazoruhusiwa Chini ya *Sera* 6

Kielelezo cha 2: Je, Vizuizi vya *Sera* Vinatumika? 9


## Akronimi na Ufupisho

| | |
|---|---|
| **DOD** | Wizara ya Ulinzi |
| **DOS** | Wizara ya Mambo ya Serikali |
| **FP** | Upangaji uzazi |
| **PEPFAR** | Mpango wa Dharura wa Rais wa Msaada wa UKIMWI |
| **PMI** | Mpango wa Rais wa Kukabiliana na Malaria |
| ***sera*** | Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa |
| **USAID** | Wakala wa Marekani wa Maendelo ya Kimataifa |
| **USG** | Serikali ya Marekani |
| **WASH** | Maji, usafi na usafi wa mwili |

# Utangulizi

Tarehe 23 Januari, 2017, Rais Trump alitia saini taarifa ya rais iliyorudisha Sera ya Jiji la Meksiko. Wakati wa utawala wa hapo awali wa chama cha Republican, sera hii ilizuia tu msaada wa serikali ya Marekani (USG) kwa upangaji uzazi na programu za afya ya uzazi. Taarifa ya 2017 ilimwelekeza waziri wa mambo ya serikali, kwa kushirikiana na waziri wa afya na huduma za binadamu, "kutekeleza mpango wa kupanua matakwa [ya sera] ... kufikia msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na wizara zote na mawakala."

Vizuizi vipya na vyenye wigo mpana vya Sera ya Jiji la Meksiko vilipewa jina jipya Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa (*sera*), ambayo wakosoaji wanaiita Sheria ya Kufunga Vinywa vya Kimataifa.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo si ya Marekani, yanayofafanuliwa kama Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zz kutengeneza faida na zisizotengeneza faida ambazo hazijapangwa chini ya sheria za Marekani, lazima zikubaliane na *sera* kama sharti la kupokea msaada wowote wa afya wa Marekani. *Sera* hii inazuia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali haya Yasiyo ya Marekani yasitekelez wala kuhamasisha uavyaji mimba kama njia ya upangaji uzazi (FP), hata kwa fedha kutoka kwenye mashirika mengine Yasiyo ya USG. Shughuli zilizozuiwa chini ya *sera* hii zinajumuisha, lakini sio tu: utunzaji baada ya kuavya mimba katika visa ambavyo si hatari kwa maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa; ushauri nasaha, ikijumuisha ushauri au taarifa, na/au rufaa za uavyaji mimba; na kushawishi watu ili kufanya uavyaji mimba uwe halali au upatikane zaidi katika nchi ya Shirika Isiyo ya Kiserikali yenyewe.**



Kwa kuongezea, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani ambayo yanakubali kufuata *sera* hii kama wapokeaji wa moja kwa moja au wapokeaji wadogo wa msaada wa afya wa Marekani hayaruhusiwi kutoa msaada wowote wa kifedha kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mengine yoyote Yasiyo ya Marekani ambayo yanatekeleza shughuli hizi.

Mashirika Yasiyo ya Kserikali Yasiyo ya Marekani yanaweza kushiriki katika aina fulani za shughuli zinazohusu uavyaji mimba na bado zistahiki msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani. Mwongozo huu unakusudia kubainisha vizuizi mahususi vilivyowekwa na *sera* hii ili kulinda na kuhifadhi utunzaji muhimu wa afya ya kuokoa maisha dhidi ya fasiri pana isiyo ya lazima kuhusu kile ambacho *sera* hii inahitaji au kukataza.

# Muhtasari wa *Sera*

Kuanzia tarehe 15 Mei, 2017, *sera* inahitaji kwamba Mashirika yote Yasiyo ya Kiserekali na Yasiyo ya Marekani yakubali na kufuata kanuni zake kama sharti la kupokea msaada wa afya wa Marekani ili kushughulikia changamoto zifuatazo za dharura za afya ya umma:

- Upangaji uzazi na afya ya uzazi;
- Uimarishaji wa mifumo ya afya;
- Mpango wa Dharura wa Rais wa Msaada wa UKIMWI (PEPFAR);
- Maji, usafi na usafi wa mwili (WASH);
- Mpango wa Rais wa Kukabiliana na Malaria (PMI);
- Afya ya mama, mtoto aliyezaliwa na mtoto;
- Magonjwa ya kitropiki yaliyotelekezwa na magonjwa mengine ya kuambukiza;
- Magonjwa Yasiyoambukizwa;
- Lishe;
- Homa tandavu ya mafua na hatari nyingine zinazoibuka, ikijumuisha usalama wa afya ulimwenguni; na
- Kifua kikuu.

Mashirika na taasisi ambazo *sera* hii haitumiki kwake zinajumuisha (angalia sehemu ya *Yasiyodhibitiwa na Sera* chini ya *Mashirika na Taasisi* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi):

- Mashirika ya kimataifa;
- Serikali ambazo si za Marekani, ingawa zinaweza kuathiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja (angalia sehemu ya *Fasiri ya Mei 2019* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi);
- Taasisi zingine za kimataifa ambazo mataifa huru hushiriki, kama vile Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana Dhidi ya UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria, na vilevile Gavi, Vaccine Alliance; na
- Mashirika Yasiyo ya Kiserekali ya Marekani.



Shughuli ambazo *sera* haitumiki kwake zinajumuisha (angalia sehemu za *Uavyaji Mimba*, *Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba* na *Utunzaji Baada ya Uavyaji Mimba* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi):

- Utunzaji wa uavyaji mimba katika visa vya hatari kwa maisha, ubakaji au ngono baina ya wanafamilia;
- Ushauri na kuelekezwa kwenye uavyaji mimba katika visa vya hatari kwa maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa; na
- Utunzaji wa baada ya uavyaji mimba, ikijumuisha "kutibu majeraha au magonjwa yanayosababishwa na uavyaji mimba halali au haramu."

Mipango mingine ya msaada wa USG ambayo *sera* hii haitumiki kwake inajumuisha (angalia sehemu ya *Wigo wa Sera* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi):

- Mpango wa Shule na Hospitali za Marekani za Ng'ambo;
- Utafiti wa msingi wa afya;
- Msaada wa Maendeleo;
- Mipango ya Vyakula kwa ajili ya Amani P.L. 480, ikijumuisha msaada wa chakula kwa madhumuni ya msaada wa dharura na maendeleo;
- Msaada wa binadamu, ikijumuisha uhamaji na usaidizi kwa wakimbizi kutoka kwenye Wizara ya Mambo ya Serikali (DOS) na shughuli za msaada wa majanga na ubinadamu kutoka kwenye Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na Wizara ya Ulinzi (DOD); na
- Matumizi ya WASH ya muundo msingi kwa ajili ya nyumba fulani, shule, vituo vya afya na matumizi ya kiviwanda na biashara, na vilevile uendelezaji wa *sera* ya kitaifa na shughuli za utawala bora.

Kumbuka kwamba pia kuna kanuni za kisheria za muda mrefu ambazo zinawekea kikomo matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserekali ya msaada wa USG kwa ajili ya shughuli zinazohusu uavyaji mimba, ikijumuisha marekebisho ya 1973 ya Helms na marekebisho ya 1981 ya Siljander. Tafadhali rejelea Kielelezo cha 1 kwa muhtasari wa shughuli zinazohusu uavyaji mimba zinazoruhusiwa chini ya *sera*. Kwa kila aina ya shughuli, kuna sehemu zinazolingana katika mwongozo huu ambazo zinaeleza wigo wa *sera* na vizuizi vyake kwa kina.

### Kielelezo cha 1: Shughuli Zinazohusiana na Uavyaji Mimba Zinazoruhusiwa Chini ya *Sera*

| Aina ya Shughuli | Mashirika Yasiyo ya | | Mashirika ya Marekani | |
|---|---|---|---|---|
| | Msaada wa USG | Msaada Usio wa USG | Msaada wa USG | Msaada Usio wa USG |
| **Uavyaji Mimba** | | | | |
| Kuavya mimba katika visa vya hatari kwa maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa | ✓ | ✓ | ★ | ★ |
| Kuavya mimba kwa sababu nyinginezo, ikijumuisha misingi mipana ya afya (kimwili na kiakili), "hitilafu za kijusi," sababu za kijamii na kiuchumi au kwa ombi | | | | ★ |
| **Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba** | | | | |
| Toa mwelekezo kuhusu uavyaji mimba, ikiwa ni halali | ⚙ | ⚙ | ✓ | ✓ |
| Toa ushauri kuhusu uavyaji mimba | | | ✓ | ✓ |
| Toa ushauri, mwelekezo na utunzaji wa kuzuia mimba baada ya uavyaji mimba | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Ushawishi Kuhusu Uavyaji Mimba** | | | | |
| Kuhamasisha serikali isiyo ya Marekani kuhalalisha au "kuendeleza uhalali" wa uavyaji mimba kwa sababu ambazo si za kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa | | | | ✓ |
| Kufanya "kampeni ya umma ya kutoa taarifa ... kuhusu faida na/au upatikanaji wa uavyaji mimba" kwa sababu ambazo si za kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa | | | | ✓ |
| **Utunzaji Baada ya Uavyaji Mimba** | | | | |
| Kununua au kusambaza vifaa vya kuvuta kijusi | | ✓ | | ✓ |
| Kufunza wafanyakazi wa afya matibabu ya matatizo ya baada ya uavyaji mimba (k.m., uavyaji mimba ambao haujakamilika au ambao umeambukizwa ugonjwa) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Kutoa msaada wa kuimarisha mifumo ya utendaji ambayo inajumuisha vifaa vya uvutaji kijusi kwa utunzaji baada ya uavyaji mimba | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Utafiti Kuhusu Uavyaji Mimba** | | | | |
| Kufanya utafiti wa biolojia ya tiba kuhusu uavyaji mimba | | + | | ✓ |
| Kujihusisha na utafiti wa kidemografia, epidemiolojia au wa sayansi ya kijamii kuhusu uavyaji mimba | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

**Tafsiri**

✓ Shughuli inayoruhusiwa chini ya marekebisho ya 1973 ya Helms, *sera* au vizuizi vingine vya kisheria na *sera* vinavyotumika.

★ Shughuli inayoruhusiwa chini ya sheria na *sera* ya sasa, lakini si wazi iwapo au mara ngapi, ikiwezekana, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani itawatunza wagonjwa bila kutegemea Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani kama mpatanishi.

⚙ Shughuli inayoruhusiwa tu chini ya hali fulani mahususi kabisa, ambazo pamoja zinafanyiza mwelekezo usio wa moja kwa moja (angalia sehemu ya *Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi).

\+ Utafiti wa aina yoyote hautajwi kihususan katika vipengele vya kawaida vinavyotekeleza *sera*. Hata hivyo, ufafanuzi wa "kuhamasisha uavyaji mimba" katika vipengele hivyo ni wa kuonyesha, si wa kina (yaani, "inajumuisha, lakini sio tu, shughuli zifuatazo"). Kuna vitu vinavyoonyesha kwamba USG inauona utafiti wa biolojia ya matibabu kuhusu uavyaji mimba unaofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, bila kujali chanzo cha fedha, kama unaifanya Shirika hilo lisilo la Kiserikali kutostahiki msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani (angalia sehemu ya *Utafi wa Mipango na Uendeshaji* chini ya *Utafiti Kuhusu Uavyaji Mimba* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi).

# Msamiati wa Kisheria wa *Sera*

Idara na mawakala wa USG, ikijumuisha USAID, DOS, Taasisi za Kitaifa za Afya, Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa na DOD, zinaongozwa na vipengele vya kawaida vinavyotekeleza *sera*.

Msamiati huu wa kisheria unazihitaji Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yakubali kwamba "hayatatekeleza au kuhamasisha uavyaji mimba kama njia ya upangaji uzazi" wala "kutoa msaada wa kifedha kwa Shirika isiyo ya Kiserikali yoyote isiyo ya Marekani ambayo inafanya shughuli hizo" wakati inapokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani.

**Uavyaji Mimba Kama Njia ya upangaji uzazi**
Kwa mujibu wa USAID, "Uavyaji mimba ni njia ya kupanga uzazi ikiwa ni kwa makusudi ya kuweka nafasi kati ya kuzaliwa kwa watoto." Hii inajumuisha, lakini sio tu, uavyaji mimba kwa ajili ya afya ya mwili na akili ya mgonjwa na unaofanywa kwa sababu ya hitilafu za kijusi. "Kuhamasisha" uavyaji mimba kama njia ya kupanga uzazi kunajumuisha, kwa mfano, ushauri wa kuavya mimba; mwelekezo, bila kujumuisha mwelekezo usio wa moja kwa moja (angalia sehemu ya *Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi); kushawishi; na kampeni za taarifa za umma.

Vipengele vya kawaida vya *sera* vimejumuishwa katika ruzuku, makubaliano ya shirika, ruzuku ndogo na ruzuku chini ya mkataba. Mnamo tarehe 14 Septemba, 2020, utawala wa Trump ulitangaza sheria iliyopendekezwa ya kuendeleza *sera* katika mikataba. Kipindi cha maelezo kitafungwa tarehe 13 Novemba, 2020. Sheria hiyo itakapokamilishwa, mikataba inayofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yatadhibitiwa na *sera* hiyo.

Marufuku za muda mrefu, kama vile marekebisho ya 1973 ya Helms na kanuni nyingine za kisheria, kuhusu matumizi ya moja kwa moja ya msaada wa USG kwa ajili ya shughuli nyingi zinazohusiana na uavyaji mimba bado zinatekelezwa.

## "Ukaguzi wa Miezi Sita"

Mnamo Februari 2018, DOS ilitoa "ukaguzi wake wa miezi sita" wa *sera* hiyo, ambayo ilipendekeza mabadiliko matatu ya kiufundi yanayofafanua vipengele vya kawaida:

1. Maana ya "kutoa msaada wa kifedha" kwa Shirika lisilo la Kiserikali lingine lolote lisilo la Marekani ambalo linafanya shughuli zinazohusu uavyaji mimba: Shirika lisilo la Kiserikali tiifu lisilo la Marekani haliwezi kulipa fedha shirika lingine ili kutekeleza shughuli ambazo zinaweza kukiuka *sera* ikiwa zinafanywa na Shirika hilo la Kiserikali hilo lenyewe lisilo la Marekani;

2. Kipengele cha kukomesha: USG ina busara ya kurekebisha na kuchukua hatua ya kusahihisha katika hali ya kufanyika kwa "kosa lisilokusudiwa" wakati mpokeaji amepatikana kukiuka *sera*, kinyume na kukomesha mara moja msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani; na

3. Matumizi ya *sera* kwa usaidizi sawia, kama vile mafunzo na msaada wa kiufundi: *Sera* hii haitumiki kwa wapokeaji na wanufaishwa wa usaidizi sawia ikiwa Shirika lisilo la Kiserikali la Marekani ambalo halijapokea tuzo au tuzo dogo la msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani.

Zaidi ya mwaka mmoja baadaye mnamo Machi 2019, utawala wa Trump ulitangaza hautapitisha pendekezo lililo hapo juu kuhusu usaidizi wa kifedha na badala yake, ukafasiri upya ibara hiyo ili kupanua wigo wa *sera* mara nyingine tena. Ingawa utawala unasisitiza kwamba "hakuna mabadiliko kwenye takwa la 'usaidizi wa kifedha' katika kipengele cha kawaida," kama ilivyoelezwa kwa kina katika barua ya tarehe 29 Mei, 2019 kutoka USAID, hii ni kweli tu kwa kadiri kwamba maandishi yenyewe hayakurekebishwa. Hata hivyo, kwa matendo, hii ni fasiri mpya ambayo inaathiri fedha zozote zinazopitia kwenye Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani inayotii *sera*.

## Vipengele vya Kawaida Vilivyorekebishwa

Mnamo Mei 2019, lugha ya vipengele vya kawaida ilirekebishwa ili kuonyesha mapendekezo hayo mawili ya baadaye yaliyofanywa katika "ukaguzi wa miezi sita." Mabadiliko hayo yanatekelezwa kwa tuzo na tuzo ndogo mpya. Lugha ya vipengele vya kawaida vilivyorekebishwa itajumuishwa katika makubaliano yaliyopo wakati Shirika zisizo za Marekani zinakabili hatua mpya ya ufadhili wa fedha inayotokea mnamo au baada ya tarehe 29 Mei, 2019. Shirika zisizo za Kiserikali za Marekani lazima zitiririshe *sera* hiyo kwa wapokeaji wadogo wa Shirika zisizo za Marekani. Shirika zisizo za Kiserikali zinaweza kuomba kurekebishwa kwa vipengele vya kawaida katika makubaliano yao wakati wowote, bila kusubiri hatua mpya ya ufadhili wa fedha.

Kuhusu ibara ya "usaidizi wa kifedha", utawala wa Trump umefasiri maneno hayo kumaanisha Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linalotii *sera* — kama mpokeaji au mpokeaji mdogo wa moja kwa moja wa msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani — imepigwa marufuku kutoa usaidizi wowote wa kifedha, bila kujali chanzo au shughuli, kwa Shirika lisilo la Kiserikali lilingine lolote lisilo la Marekani ambalo linaendesha shughuli zilizopigwa marufuku chini ya *sera*. Ikiwa Shirika hilo lisilo la Kiserikali hilo lisilo la Marekani litatoa "usaidizi wa kifedha" kwa Shirika lisilo la Kiserikali linguine lisilo la Marekani linalojishughulisha na shughuli za uavyaji mimba zilizopigwa marufuku, yenyewe itafanya isistahiki kupokea msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani. Kufikia Mei 2019, takwa hilo linatumika kwa mipango ya kifedha iliyopo ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, isipokuwa Shirika hilo lisilo la Kiserikali liwe lina jukumu la kisheria la kuandaa fedha za ziada chini ya mpango huo.

# Wakati wa Kutekelezwa

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani ambayo yanapokea msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani lazima yahakikishe kuwa yanatii *sera* mara tu yanapokubali vipengele vya kawaida katika tuzo au tuzo ndogo (ruzuku, makubaliano ya shirika, ruzuku ndogo na ruzuku chini ya mkataba) ili kupokea msaada wa USG.

Hii itafanyika wakati Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanakabili hatua mpya ya kifedha mnamo au baada ya tarehe 15 Mei, 2017, kupitia tuzo mpya au wakati ruzuku iliyopo, makubaliano ya shirika, ruzuku ndogo au ruzuku chini ya mkataba inarekebishwa “ili kuongeza fedha za ziada” au “ili kuongeza fedha mpya.” Vizuizi hivyo havitumiki kwa fedha ambazo tayari zimejukumiwa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani — kama mpokeaji au mpokeaji mdogo — chini ya ruzuku iliyopo, makubaliano ya shirika, ruzuku ndogo au ruzuku chini ya mkataba hadi shirika husika likubali kutii *sera*, na wakati huo itatumika kwa fedha zote zilizopo.

Si lazima Shirika lisilo la Kiserikali la Marekani litiririshe chini *sera* hiyo kwa wapokeaji wake wadogo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani hadi Shirika hilo lisilo la Kiserikali la Marekani likubali vipengele vya kawaida katika makubaliano yake yenyewe pamoja na USG. Kama ilivyo kwa Mashirika mengine yasiyz ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, hii itafanyika wakati Shirika hilo lisilo la Kiserikali la Marekani itakabili hatua mpya ya kifedha, katika majadiliano ya tuzo mpya au wakati ruzuku iliyopo, makubaliano ya shirika, ruzuku dogo au ruzuku chini ya mkataba inarekebishwa “ili kuongeza fedha za ziada” au “ili kuongeza fedha mpya.”

Shirika lisilo la Kiserikali huonyesha ridhaa yao ya kufuata masharti ya *sera* kwa kukubali vipengele vya kawaida katika tuzo zao. Hakuna vyeti tofauti vinavyohitajika.

### Fasiri ya Mei 2019

Baada ya Mei 2019, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani ambayo yanatii *sera* lazima yahakikishe wapokeaji wao wadogo pia wanatii kabla ya kutoa usaidizi wa kifedha zikitumia fedha zao wenyewe tofauti na tuzo zao za msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani.

Fasiri ya Mei 2019 inaathiri msaada wa afya wa kimataifa usio wa Marekani na vyanzo vya kifedha visivyo vya USG, ikijumuisha fedha kutoka kwa wafadhili wengine wa kimataifa wasio wa Marekani, taasisi za kibinafsi na vyanzo vingine vya fedha vya USG vilivyo nje ya afya ya kimataifa. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanayotii *sera* lazima sasa zitekeleze “uangalifu unaofaa” kwa wapokeaji wadogo wao wowote au wote, bila kujali chanzo cha fedha na chanzo cha shughuli, ili kuhakikisha hawajihusishi katika shughuli zozote zilizopigwa marufuku na *sera*.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanayotii yanapaswa kutambua fasiri hiyo inatumika kwenye “usaidizi wa kifedha” unaoanza baada ya Mei 2019. Bila kujali fasiri hii, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanaweza kujipata yakiwa yamefungwa kisheria na makubaliano yaliyopo ya kuendelea kutoa “usaidizi wa kifedha” au yakabiliwe na athari za kisheria au kifedha.

# Wigo wa *Sera*

**Kielelezo cha 2: Je, Vizuizi vya *Sera* Vinatumika?**

| NDIYO | LA |
|---|---|
| **Mashirika na Taasisi** | |
| • Shirika zisizo za Marekani, zinazotengeneza faida na zisizotengeneza faida<br>• Shirika zisizo za Marekani ambazo ni wapokeaji wadogo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani zinazotii *sera* (bila kujali chanzo wala shughuli) au Shrika lisilo la Kiserikali la Marekani inayopokea msaada wa afya wa kimataifa Marekani | • Gavi, Vaccine Alliance<br>• Mashirika ya kimataifa<br>• Serikali ambazo si za Marekani<br>• Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria<br>• Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani |
| **Bajeti au Akaunti za Mchanganuo** | |
| • Msaada kwa Ulaya Mashariki, Eurasia na Asia ya Kati<br>• Fedha za Usaidizi wa Kiuchumi<br>• Mipango ya Afya ya Kimataifa<br>• PEPFAR | • Msaada wa Maendeleo<br>• Vyakula kwa ajili ya Amani P.L. 480 Title II Grants<br>• Msaada wa Majanga ya Kimataifa<br>• Msaada wa Uhamaji na Wakimbizi<br>• Mfuko wa Marekani wa Msaada wa Dharura wa Uhamaji na Wakimbizi |
| **Vyombo vya Msaada** | |
| • Mikataba (ikisubiri ukamilishaji wa sheria iliyopendekezwa)<br>• Makubaliano ya shirika<br>• Ruzuku na ruzuku ndogo<br>• Ruzuku chini ya mikataba | • Ruzuku ndogo kutoka kwa serikali isiyo ya Marekani<br>• Maagizo ya manunuzi kwa bidhaa na huduma ambazo hazihusiani moja kwa moja na utoaji wa msaada wa afya wa kimataifa (k.m., usafirishaji) |
| **Mipango ya Msaada*** | |
| • Kupanga uzazi na afya ya uzazi<br>• VVU/UKIMWI, ikijumuisha PEPFAR<br>• Malaria, ikijumuisha PMI<br>• Afya ya mama na mtoto, ikijumuisha WASH kwenye kiwango cha jumuiya na familia<br>• Lishe<br>• Hatari nyingine za afya ya umma, ikijumuisha magonjwa ya kitropiki yaliyotelekezwa na magonjwa mengine ya kuambukizwa, magonjwa Yasiyoambukizwa na uimarishaji wa mfumo wa afya<br>• Homa tandavu ya mafua na hatari zingine zinazoibuka, ikijumuisha usalama wa afya ulimwenguni<br>• Kifua kikuu | • Mpango wa Shule na Hospitali za Marekani Zilizo Ng'ambo<br>• Msaada wa Maendeleo, ikijumuisha miundo mbinu na huduma za maji na usafi<br>• Msaada wa ubinadamu, ikijumuisha msaada wa DOS wa uhamaji na wakimbizi na vilevile msaada wa majanga na ubinadamu wa USAID na DOD<br>• Msaada wa chakula P.L. 480 |
| **Aina ya Misaada na Usaidizi** | |
| • Bidhaa<br>• Vifaa<br>• Ushirika<br>• Fedha<br>• Msaada wa kiufundi<br>• Mafunzo (mengi — hasa kama yanaimarisha uwezo wa kishirika) | • Mikopo<br>• Maingiliano ya muda mfupi (k.m., mashauriano, mahojiano, ukusanyaji wa data au machapisho)<br>• Bidhaa au huduma za kununuliwa (k.m., kompyuta, usimamizi au bidhaa za ofisi) |
| **Watu Binafsi Wanaopokea Msaada** | |
| • Mtu anayeshirikiana na anayetenda kwa jina la Shirika hilo<br>• Watu wanaoshirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali wanaoshiriki katika mafunzo mahususi | • Watu wanaoshirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wanaotenda kwa niaba yao wenyewe<br>• Watu wanaoshirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wanaoshiriki katika "mpango wa jumla wa mafunzo" |

* *Angalia Wizara ya Mambo ya Serikali ya Marekani, Ofisi ya Utawala, Ofisi ya Mtendaji wa Manunuzi (2017), Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa, Msaada wa Serikali Kuu wa Usimamizi wa Ushauri Namba 2017-01, na kategoria ya afya chini ya Mpango wa Kawaida wa Msaada wa Kigeni kwenye* https://www.state.gov/f/releases/other/255986.htm#HL.

## Mashirika na Taasisi

### Yanayodhibitiwa na *Sera*

Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani inayopokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani — kupitia tume ya nchi ya USG, wakala anayeshirikiana wa Marekani, Shirika lisilo la Kiserikali la Marekani au Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linalotoa fedha kwa wapokeaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani — linapaswa kutathmini kwa kina ruzuku yoyote, makubaliano ya shirika, ruzuku ndogo au ruzuku chini ya mkataba ili kutambua iwapo *sera* hiyo ni sheria au sharti la ufadhili wa fedha. Ikiwa ndivyo, Shirika hilo lisilo la Kiserikali hiyo na lisilo la Marekani litakuwa na jukumu la kushikamana na vizuizi vya *sera* katika mipango yake yote, bila kujali chanzo cha ufadhili wa kifedha. Msaada unafafanuliwa kujumuisha sio fedha tu, bali utoaji wa bidhaa na vifaa.

Mnamo tarehe 14 Septemba, 2020, utawala wa Trump ulitangaza sheria iliyopendekezwa ya kuendeleza *sera* katika mikataba. Kipindi cha maelezo kitafungwa tarehe 13 Novemba, 2020. Sheria hiyo itakapokamilishwa, mikataba inayofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yatadhibitiwa na *sera* na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yatahitaji kuanza kukagua kwa kina makubaliano yao ya kimkataba ili kutambua iwapo *sera* ni sheria na sharti la ufadhili huo wa fedha.

*Sera* ina takwa la mtiririko wa kwenda chini tu. Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani — hata lile ambalo limekubali kutii *sera* — haihatarishi ustahiki wake yenyewe wa msaada wa afya ya kimataifa Marekani kwa kuwa mpokeaji mdogo wa fedha kutoka kwa Shirika lisilo la Kiserikali lingine lisilo la Marekani ambalo limechagua kutofungwa na kutofungwa na *sera*, maadamu mpokeaji mdogo huyo hatumii fedha hizo kujihusisha katika shughuli zozote zilizopigwa marufuku na *sera*.

### Yasiyodhibitiwa na *Sera*

#### Mashirika

Shirika lisilo la Kiserikali lisilo lisilo la Marekani halihitajiki kukubali *sera* ikiwa linapokea tu msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani kama muuzaji wa bidhaa au huduma (k.m., usaidizi wa kompyuta, usimamizi au bidhaa za ofisi) kwa mpokeaji mkuu au mpokeaji mdogo wa fedha hizo za USG.



Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani yanaweza kuendelea kutekeleza, kutoa ushauri, kuelekeza au kufanya utetezi kuhusu uavyaji mimba na fedha kutoka kwenye vyanzo visivyo vya USG bila kuhatarisha ustahiki wa kupokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani. Takwa pekee lililowekwa kwa Mashirika haya Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani ni jukumu la kutiririsha chini *sera* hiyo kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, ambayo ni wapokeaji wadogo wa msaada wa afya ya kimataifa Marekani.

#### Wafanyakazi wa Mashirika

Vizuizi vya *sera* vinatumika kwa mashirika, sio watu binafsi. Mtu anayejihusisha na Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linalodhibitiwa na *sera* anaweza kujihusisha, kama mtu binafsi, na shughuli ambazo zingepigwa marufuku ikiwa zingetekelezwa na shirika lenyewe. Mtu anaweza kujihusisha na shughuli hizi ambazo vinginevyo zimezuiwa maadamu "hayupo kazini au hatendi akiwa katika eneo la kazi la shirika hilo," shirika hilo haliungi mkono au kufadhili hatua hiyo na "hatua zifaazo" zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa mtu huyo "hajiwakilishi isivyofaa" kwamba anatenda kwa niaba ya shirika hilo (angalia sehemu ya *Mafunzo na Vifaa* chini ya *Utunzaji Baada ya Uavyaji Mimba* na *Msaada wa Kiufundi* katika mwongozo huu kwa maelezo zaidi).

#### Serikali Ambazo Si za Marekani

Huduma za afya zinazotolewa chini ya ufadhili wa serikali za kitaifa na serikali ndogo zisizo za Marekani na mashirika ya umma ya kimataifa, ikijumuisha utunzaji wa afya unaotolewa katika sekta ya umma, hazidhibitiwi na *sera*. Ikiwa mipango ya sekta ya umma inatoa uavyaji mimba kama njia ya kupanga uzazi au kujihusisha katika shughuli zingine zinazohusiana na uavyaji mimba ambazo zimepigwa marufuku, serikali na mashirika yanahitajiwa kuweka msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani katika akaunti tofauti ili kuhakikisha kwamba fedha za USG hazitumiwi kwenye shughuli hizi zilizopigwa marufuku. Vifaa vya matibabu vilivyonunuliwa kwa fedha za USG na vituo vinavyosaidiwa na USG haviwezi kutumiwa kutoa utunzaji wa uavyaji mimba wa kukusudiwa. Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linalotoa msaada kwa sekta ya umma bado linadhibitiwa na *sera* ikiwa inapokea msaada wa afya ya kimataifa Marekani.

Msamaha kwa serikali zisizo za Marekani pia unatumika kwa vyuo vikuu na hospitali zinazoendeshwa na serikali, ikijumuisha shule za tiba na hospitali za mafunzo ambazo hutoa utunzaji wa uavyaji mimba kama sehemu ya huduma za afya za kina au kujihusisha katika utafiti unaohusiana na uavyaji mimba.

Msamaha huo pia unatumika kwa mabaraza ya ushauri wa afya yanayodhaminiwa na serikali, ambayo yako huru kushiriki katika utafiti; kusambaza taarifa za umma kuhusu kuenea, visababishi au athari za uavyaji mimba usio salama; na kushiriki katika uendelezaji wa *sera* za eneo zinazohusu uavyaji mimba.

Kufuatia fasiri ya Mei 2019, Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani ambalo linatii *sera* lazima litumie uangalifu unaofaa kwa wapokeaji wake wadogo ili kuhakikisha utii huohuo kabla ya kutoa usaidizi wowote wa kifedha ambao Shirika lisilo la Kiserikali hilo limepokea kutoka kwa serikali ambazo si za Marekani. Hata hivyo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanaweza kujipata yakiwa yamefungwa kisheria na makubaliano yaliyopo ya kuendelea kutoa "usaidizi wa kifedha" au zikabiliwe na athari za kisheria au kifedha.

#### Mashirika Ya Kimataifa

Mashirika ya kimataifa au ya umma kama vile Shirika la Afya Duniani, Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa Kuhusu VVU/UKIMWI na UNICEF, na vilevile "taasisi zingine za kimataifa ambamo mataifa huru yanashiriki (kama vile Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, na vilevile Gavi, Vaccine Alliance),' hayadhibitiwi na *sera*.

Kufikia Mei 2019, Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani ambalo linatii *sera* lazima liwe na uangalifu unaofaa kwa wapokeaji wake wadogo ili kuhakikisha utii huohuo kabla ya kutoa usaidizi wowote wa kifedha ambao Shirika lisilo la Kiserikali hilo limepokea kutoka kwa mashirika ya kimataifa au ya umma.

## Shughuli

### Uavyaji Mimba

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani bado yanastahiki msaada wa afya ya kimataifa Marekani ikiwa yanafanya uavyaji mimba katika visa ambapo "maisha ya mama yatahatarishwa iwapo kijusi kitaendelea hadi kuzaliwa" au "baada ya kubakwa au ngono kutoka kwa mtu wa jamaa." Chini ya masharti ya *sera*, uavyaji mimba unaofanywa kwa sababu nyingine yoyote au hali ni marufuku, ikijumuisha "afya ya mwili na akili ya mama na uavyaji mimba unaofanywa kwa sababu ya hitilafu za kijusi."

Hata hivyo, iwapo Shirika isiyo ya Marekani inayopokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani inafanya uavyaji mimba katika hali ya kuhatarisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa — hata ingawa imeruhusiwa moja kwa moja na *sera* — Shirika hilo linapaswa kufikiria kurekodi hali na sababu za hatua hiyo ili kuonyesha waziwazi utiifu wa *sera* na matakwa ya sheria za eneo kwa ajili ya rekodi zake yenyewe.

Shirika lisilo la Marekani haliondolewi kwenye msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani ikiwa inamiliki vifaa vya kuvuta kijusi, vyombo vya kupanua na kukwangua tishu; na/au dawa za kuchochea hedhi, kwa hali za kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa au ili kutibu matatizo ya kuharibika kwa mimba au kutokana na uavyaji mimba Hata hivyo, msaada wa afya ya kimataifa Marekani hauwezi kutumiwa kununua au kusambaza vifaa hivyo.

### Ushauri na Kuelekezwa katika Kuavya Mimba

Ushauri na mwelekezo wa uavyaji mimba zinaruhusiwa katika visa vya hatari kwa maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa.

Katika nchi ambapo uavyaji mimba ni halali kwa sababu ambazo ni zaidi ya kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa, mawasiliano ya wazi kati ya wagonjwa na watoa huduma za afya yamezuiwa kabisa na *sera*. Mwelekezo usio wa moja kwa moja kwa ajili ya uavyaji mimba unaruhusiwa katika nchi hizo ikiwa tu hali zote nne zifuatazo zimekidhiwa:

- Mgonjwa tayari ni mjamzito;
- Mgonjwa "anasema waziwazi kwamba tayari ameamua" kuavya mimba;
- Mgonjwa "anauliza hususan" mahali ambapo uavyaji mimba salama na halali unaweza kupatikana; na
- Mtoa huduma za afya ana sababu ya kuamini kwamba maadili ya tiba ya nchi yanahitaji mwelekezo kwa ajili ya uavyaji mimba salama na halali.

*Sera* inajumuisha msamaha mmoja wa ziada kwa vizuizi juu ya ushauri na mwelekezo kwa ajili ya kuavya mimba. Shirika isiyo ya Marekani haitahatarisha ustahiki wake wa kupata msaada wa afya ya kimataifa Marekani ikiwa kuna "jukumu la mtoa huduma za afya" linalomhitaji mtoa huduma huyo chini ya sheria ya eneo kutoa ushauri na mwelekezo kwa ajili ya uavyaji mimba kwa sababu ambazo hazihusu kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa. Matumizi mapana ya msamaha huu yanaonekana kutiliwa shaka na kutegemea vipengele ambavyo pengine vipo katika sheria za eneo. Hata hivyo, Mashirika Yasiyo ya Marekani yanahimizwa kutafuta ushauri moja kwa moja kutoka kwa idara ya USG au wakala anayetoa msaada huo na/au washirika watekelezaji wengine wa USG katika nchi hiyo ili kutambua ikiwa msamaha huu unatumika katika hali za eneo lao.

### Ushawishi Kuhusu Uavyaji Mimba

Shirika zisizo za Marekani ambazo zinapokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani hazipaswi kuhamasisha serikali yao "kuendeleza uhalali" wa uavyaji mimba kwa sababu ambazo si za kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa.

Aidha, Shirika zisizo za Marekani zinazopokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani hazipaswi kuendesha "kampeni ya taarifa ya umma … kuhusu faida na/au upatikanaji wa uavyaji mimba" isipokuwa katika visa vya kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa. Hata hivyo, *sera* haizuii matumizi ya demografia na utafiti wa afya kuhusu uavyaji mimba unaofanywa na Shirika fulani — kama vile Shirika ya Marekani au Shirika isiyo ya Marekani ambayo haipokei msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani — ili kuhamasisha serikali zisizo za Marekani ili kuhalalisha uavyaji mimba.

Kumbuka kwamba matumizi ya msaada wa USG ili "kutetea au kupinga" uavyaji mimba yamepigwa marufuku chini ya marekebisho ya 1981 ya Siljander.

### Utunzaji Baada ya Uavyaji Mimba

#### Mafunzo na Vifaa

*Sera* inaziruhusu waziwazi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani "matibabu ya majeraha au magonjwa yanayosababishwa na uavyaji mimba halali au usio halali, kwa mfano, utunzaji baada ya kuavya mimba." Mashirika yanahimizwa kutoa matibabu ya athari za baada ya uavyaji mimba (k.m., uavyaji mimba usiokamilika au ulioambukiza ugonjwa) yenyewe au kuwasaidia wagonjwa kupata matibabu (k.m., kwa kuandamana na mgonjwa kwenda hospitali).

Msaada wa USAID unaweza kutumiwa kusaidia mafunzo ya wafanyakazi wa afya ya utunzaji baada ya kuavya mimba, matibabu yenyewe na msaada mwingine husika wa kiufundi. Lakini kama *sera* ya wakala, fedha za USAID haziwezi kutumiwa kununua vifaa vya kuvuta kijusi au dawa zingine za kutoa utunzaji baada ya kuavya mimba. Hata hivyo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hayazuiwi kutumia fedha zisizo za USG kutimiza matakwa ya kugawana gharama ya USAID ya kununua vifaa vya kuvuta kijusi au bidhaa nyingine kwa makusudi ya utunzaji baada ya kuavya mimba.

#### Ushauri na Huduma za Kuzuia Mimba

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaweza kupokea na kutumia msaada wa afya ya kimataifa Marekani kutoa nasaha na huduma za kuzuia mimba kwa wagonjwa ambao wamekabili kuharibika kwa mimba au uavyaji mimba, ikijumuisha uavyaji mimba usio halali. Mashirika yanaweza kuwasiliana na kuratibu shughuli na Mashirika mengine Yasiyo ya Kiserikali yoyote isiyo ya Marekani, ikijumuisha watoa huduma za uavyaji mimba, ili kuwezesha utunzaji wa kuzuia mimba au afya ya uzazi.

### Kutoa Huduma Za Kuzuia Mimba

*Sera* haizuii Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani kutoa njia yoyote iliyopo ya kuzuia mimba iliyoidhinishwa na shirika la Marekani la Usimamizi wa Chakula na Dawa, ikijumuisha dawa za dharura za kuzuia mimba. Mashirika yote Yasiyo ya Kiserikali yanayopokea msaada wa afya ya kimataifa wa Marekani zinaweza kutoa ushauri wa kuzuia mimba, kutoa bidhaa za kuzuia mimba na kuhamasisha uelewa wa njia za kuzuia mimba kwa mujibu wa sheria na *sera* za eneo.

### Utafiti Kuhusu Uavyaji Mimba

#### Utafiti wa Tiba ya Biolojia

Chini ya marufuku ya sheria ya 1981 iliyotungwa na bunge la Marekani, mashirika — Mashirika ya Marekani na Yasiyo ya Marekani — hayawezi kutumia fedha za USG kushiriki katika utafiti wa tiba ya biolojia kuhusu uavyaji mimba. Hata hivyo, Mashirika ya Marekani yanaweza kutumia fedha zilizopatikana kutoka vyanzo vingine kufanya utafiti huo.

Utafiti wa aina yoyote hautajwi kihususan katika vipengele vya kawaida vinavyotekeleza *sera*. Hata hivyo, ufafanuzi wa "kuhamasisha uavyaji mimba" katika vipengele hivyo ni wa kuonyesha, si wa kina (yaani, "inajumuisha, lakini sio tu, shughuli zilizo hapo juu"). Kuna vitu vinavyoonyesha kwamba USG inauona utafiti wa biolojia ya tiba kuhusu uavyaji mimba unaofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, bila kujali chanzo cha fedha, kama unaifanya Shirika hilo hiyo kutostahiki msaada wa afya wa kimataifa Marekani.

#### Utafiti wa Kidemografia na Afya

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Yasiyo ya Marekani hayahatarishi ustahiki wao wa kupata msaada wa afya ya kimataifa Marekani ikiwa zitashiriki katika aina fulani za utafiti wa uavyaji mimba. Mbali na kuweka taarifa za kawaida kuhusu historia ya uavyaji mimba ya wagonjwa, mashirika yanaweza kukusanya taarifa kuhusu kuenea kwa jumla kwa uavyaji mimba na sababu zake; athari za kiafya za uavyaji mimba usio halali, ikijumuisha vifo na majeraha yanayohusiana nazo; na gharama zake kwa mfumo wa utoaji wa utunzaji wa afya. Aina hizi za utafiti wa epidemolojia au maelezo unaweza kusaidiwa na fedha za USG.

Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linalopokea msaada wa afya ya kimataifa Marekani haipaswi kutumia matokeo ya utafiti huu — bila kujali iwapo utafiti huo unafadhiliwa na USG — au utafiti mwingine wowote ili kutetea au kuendesha kampeni ya taarifa ya umma kwa ajili ya kuhalalisha uavyaji mimba au kuendeleza sheria za uavyaji mimba isipokuwa katika visa vinavyozidi kuhatarisha maisha, ubakaji au ngono baina ya watu wa jamaa. Lakini ustahiki wa Shirika hilo lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani wa kupata msaada wa afya ya kimataifa Marekani hauhatarishwi kwa kushiriki tu katika utafiti ambao huenda wengine wakautumia katika kuendeleza marekebisho ya sheria ya uavyaji mimba. Aidha, Shirika hilo lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linaruhusiwa kusambaza hadharani utafiti wa kidemografia na afya kuhusu uavyaji mimba maadamu haitumii matokeo hayo ili kupendekeza ulegezaji wa sheria za uavyaji mimba (k.m., katika makala ya majarida au machapisho mengine ambayo Shirika hilo lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani linaweza lenyewe kutoa na kusambaza).

#### Utafiti wa Mipango na Uendeshaji

Ingawa utafiti wa mipango na uendeshaji kuhusu uavyaji mimba haujajumuishwa waziwazi au kufafanuliwa katika vipengele vya kawaida vilivyojumuishwa katika *sera*, DOS imetoa mwongozo wa vyombo vya habari kuhusu utafiti huu. Mwongozo huo unasema kwamba Shirika lisilo la Kiserikali lisilo la Marekani ambalo linajihusisha katika "kutekeleza utafiti wa sayansi, utafiti wa uendeshaji au mipango, tathmini ya mahitaji na uimarishaji husika wa uwezo unaoendeshwa kwa madhumuni ya kuboresha mipango ya msaada wa afya ya kimataifa inayofadhiliwa na serikali ya Marekani lazima ikubali kipengele hicho katika makubaliano yao ili kupokea msaada wa afya ya kimataifa Marekani.

### Msaada wa Kiufundi

Mnamo Mei 2019, vipengele vya kawaida vilirekebishwa ili kufafanua kwamba matakwa ya *sera* hayatumiki kwa wapokeaji wa mafunzo ya mabadilishano na msaada wa kiufundi ikiwa hao ni Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani ambayo hayajapokea tuzo au tuzo dogo la msaada wa afya ya kimataifa Marekani.



## Majukumu ya Utiifu na Ufuatiliaji

Ikiwa Shirika lisilo la Kiserikali la Marekani linalopokea msaada wa afya ya kimataifa Marekani inatoa ufadhili wa fedha kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani, linawajibika kutiririsha chini *sera* na kufuatilia utiifu wao. Shirika lisilo la Kiserikali lina jukumu la kuhakikisha linatii linapopokea msaada wa afya ya kimataifa Marekani moja kwa moja kutoka USG, na pia ni lazima itiririshe chini *sera* na kufuatilia utiifu wa washirika wengine wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani kutoka kwenye shirika husika kama wapokeaji wadogo. Hati ya USAID (2019) ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara na majibu inasema:

> Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanaweza kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha utiifu wa takwa la "usaidizi wa kifedha." Uangalifu huu unaofaa unaweza kujumuisha, kwa mfano, kukutana na wapokeaji wa fedha na kukagua taarifa zinazopatikana kwa umma kuhusu shughuli zao. Wapokeaji wana jukumu la kuamua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha utiifu wa kipengele cha kawaida.

Hatua za kuhakikisha utiifu zinaweza kujumuisha:

- Uendelezaji wa taratibu za kukagua Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani wakati wa hatua ya awali ya pendekezo la uendelezaji;
- Kuthibitisha ustahiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani kupata msaada wa afya ya kimataifa Marekani na ukubalifu wa kutii *sera* kwa kujumuisha vipengele vya kawaida vinavyotekeleza *sera* katika makubaliano ya mwisho, yaliyotiwa sahihi;
- Utekelezaji wa tathmini za uangalifu unaofaa ili kuhakikisha kwamba Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani yanatii *sera*;
- Ukaguzi wa kuhakikisha utiifu kwa msingi wa kuendelea mara mradi utakapokuwa umeanza, ikijumuisha kupitia shughuli kama vile ziara za nyanjani zinazofanywa na wafanyakazi wa ndani ya nchi, kanda na makao makuu, matumizi ya orodha kaguzi za utiifu na/au kuripoti utiifu katika ripoti za maendeleo ya mradi;
- Kuwaelimisha na kuwafunza wafanyakazi kuhusu *sera*, ikijumuisha kutengeneza miongozo na vifaa vingine vya taarifa; na
- Kutengeneza itifaki za kishirika kwa ajili ya kutambua ukiukwaji unaoshukiwa na kuchukua hatua ya kurekebisha.

Kwa ufafanuzi rasmi wa vizuizi vya *sera* vinavyoathiri msaada wa afya ya kimataifa Marekani, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kutafuta ushauri moja kwa moja kutoka kwa idara ya USG au wakala anayetoa msaada huo. Hii inajumuisha mawasiliano na wafanyakazi katika ofisi za nyanjani na makao makuu ya Washington, D.C. Ili kuamua utumikaji wa *sera* kwenye shughuli zao zisizofadhiliwa na USG, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kushauriana na wafadhili wao ambao si USG na makubaliano ya ufadhili wa fedha.

# Taarifa Zaidi

**Kwa tangazo la kwanza la *sera* na mawasiliano kutoka USG, tembelea:**

- Trump, D. (2017, Januari 23). Presidential Memorandum Regarding the Mexico City Policy [Mkataba wa Rais Kuhusu Sera ya Jiji la Meksiko]. *The White House*. https://www.whitehouse.gov/presidential-actions/presidential-memorandum-regarding-mexico-city-policy
- Idara ya Jimbo la Marekani, Ofisi ya Idadi ya Watu, Wakimbizi, na Uhamiaji. (2017, Mei 15). Implementation of Protecting Life in Global Health Assistance (Formerly known as the 'Mexico City Policy') [Utekelezaji wa Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani (Zamani ilijulikana kama 'Sera ya Jiji la Meksiko')]. https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/FINAL-MCP-Press-Guidance_2017-05-14.pdf

**Kwa maandishi kamili ya vifungu vya kawaida ambavyo vinafaa kuingizwa katika makubaliano ya usaidizi wa afya ya kimataifa ya Marekani kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na idara zingine za USG na wakala, tembelea:**

- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2019, Mei). Protecting Life in Global Health Assistance (May 2019). In standard Provisions for U.S. Nongovernmental Organizations [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani (Mei 2019). Katika Masharti ya Kawaida kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Marekani] (uk.77-87). https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/1868/303maa.pdf
- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2019, Mei). Protecting Life in Global Health Assistance (May 2019). In standard Provisions for U.S. Nongovernmental Organizations [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani (Mei 2019). Katika Masharti ya Kawaida kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yasiyo ya Marekani] (uk. 87-98). https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/303mab.pdf
- Idara ya Jimbo la Marekani. (2019, Aprili). Protecting Life in Global Health Assistance (April 2019) [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani (Aprili 2019)]. https://www.state.gov/wp-content/uploads/2019/05/Protecting-Life-in-Global-Health-Assistance-Award-Provision.pdf
- Taasisi za Kitaifa za Afya. (2019, Februari 20). Protecting Life in Global Health Assistance [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani]. https://grants.nih.gov/policy/protecting-life-global-health-assistance.htm
- Vituo vya Udhibiti na Kuzuia Magonjwa. (2017, Mei). HHS Standard Provision: Protecting Life in Global Health Assistance (May 2017) [Kipengele cha Kawaida cha HHS: Msaada wa Kulinda Maisha Katika Afya ya Kimataifa (Mei 2017)]. https://www.cdc.gov/grants/additionalrequirements/ar-35.html

**Kwa ujumbe wa ndani kutoka USG kuhusu utekelezaji wa *sera*, tembelea:**

- Idara ya Jimbo la Marekani, Ofisi ya Utawala, Ofisi ya Mtendaji wa Ununuzi. (2017, Mei 15). Protecting Life in Global Health Assistance. Federal Assistance Management Advisory Number 2017-01 [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani. Nambari ya Ushauri ya Usimamizi wa Shirikisho 2017-01]. https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/FAMA-2017_01-Protecting-Life-in-Global-Health-Assistance.pdf
- Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa. (2017, Mei 15). Implementation of Protecting Life in Global Health Assistance (Formerly known as the 'The Mexico City Policy') [Utekelezaji wa Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Ulimwenguni (zamani ulijulikana kama Sera ya Jiji la Meksiko)]. USAID/Ilani ya Jumla. https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/Implementation-of-Protecting-Life-in-Global-Health-Assistance_USAIDGeneral-Notice.pdf
- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2019, Mei 29). Barua kwa washirika wa kutekeleza. https://pai.org/wp-content/uploads/2020/09/PLGHA-Partner-Letter-May-2019.pdf

**Kwa kila badiliko kwenye *sera*, ikijumuisha tathmini za USG, tembelea:**

- Idara ya Jimbo la Marekani. (2018, Februari 6). Protecting Life in Global Health Assistance Six-Month Review [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani Mapitio ya Miezi Sita]. https://www.state.gov/protecting-life-in-global-health-assistance-six-month-review
- Idara ya Jimbo la Marekani. (2019, Machi 26). Maneno kwa Wanahabari. Michael R. Pompeo, Katibu wa Jimbo. https://www.state.gov/remarks-to-the-press-7
- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2019, Oktoba). Protecting Life in Global Health Assistance Frequently Asked Questions and Answers [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Ulimwenguni Maswali na Majibu Yanayoulizwa Mara kwa Mara]. https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/1864/FINAL_Protecting_Life_in_Global_Health_Assistance_FAQs_Oct_2019_USAID.pdf
- Idara ya Jimbo la Marekani. (2020, Agosti 18). Review of the Implementation of the Protecting Life in Global Health Assistance Policy [Marudio ya Utekelezaji wa Kulinda Maisha katika Sera ya Msaada wa Afya Ulimwenguni]. https://www.state.gov/wp-content/uploads/2020/08/PLGHA-2019-Review-Final-8.17.2020-508.pdf
- Idara ya Ulinzi ya Marekani, Utawala Mkuu wa Huduma, na Anga ya Kitaifa na Utawala wa Anga. (2020, Septemba 14). Federal Acquisition Regulation: Protecting Life in Global Health Assistance [Kanuni ya Upataji wa Shirikisho: Kulinda Maisha katika Msaada wa Kiafya wa Ulimwenguni]. *Federal Register*. https://www.federalregister.gov/documents/2020/09/14/2020-17551/federal-acquisition-regulation-protecting-life-in-global-health-assistance

### Kwa vizuizi vya sasa vya sheria na *sera* juu ya msaada wa USG unaohusu uavyaji mimba, tembelea:

- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2020, Septemba 9). Global Health Legislative & Policy Requirements: Restrictions on Support for Abortions [Masharti ya Ubunge na Afya ya Ulimwenguni: Vizuizi juu ya Msaada wa Kutoa Mimba]. https://www.usaid.gov/global-health/legislative-policy-requirements

### Kwa kujitolea na ulinzi wa chaguo sahihi, tembelea:

- Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa. (2019, Juni 2). Global Health Legislative & Policy Requirements: Restrictions on Support for Abortions [Kujitolea na Chaguo sahihi]. https://www.usaid.gov/global-health/health-areas/family-planning/voluntarism-and-informed-choice

### Kwa Udhibitisho wa Kituo cha Afya cha Ulimwenguni juu ya *sera*, tembelea:

- Kituo cha Mafunzo ya Afya Duniani. (2020, Januari 6). Protecting Life in Global Health Assistance and Statutory Abortion Restrictions – 2020 [Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya Duniani na Vizuizi Vya Uavyaji Mimba - 2020]. https://www.globalhealthlearning.org/course/protecting-life-global-health-assistance-and-statutory
- Kituo cha Mafunzo ya Afya Duniani. (2020, Januari 6). US Abortion and FP Requirements – 2020 [Masharti ya Utoaji mimba Marekani na masharti ya FP – 2020]. https://www.globalhealthlearning.org/course/us-abortion-and-fp-requirements-2020
- Kituo cha Mafunzo Mtandaoni ya Afya Duniani. (2020, Januari 6). HIV/AIDS Legal and Policy Requirements [Masharti ya Sheria na Sera ya VVU/UKIMWI]. https://www.globalhealthlearning.org/course/hiv-aids-legal-and-policy-requirements



PAI

pai.org

1300 barabara ya 19 NW, Jumba la 200 | Washington, DC 20036 | +1 (202) 557-3400 | info@pai.org | www.pai.org

@pai_org | @paiwdc | @pai_org